Tanzu ni istilahi inayotumiwa kuelezea au kurejelea aina mbalimbali za kifasihi. Inawezekana utanzu mkuu kuwa na vitanzu vingine mablimbali kwa mfano, tanzu kuu za kifasihi Riwaya, Tamthiliya, shairi, Novela Insha na hadithi Wamitila (2003).

Wamitila K. W (2003), Kamusi ya fasihi istilahi za nadharia, focus Publications Ltd.
Mulokozi (1996) Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili. TUKI. Dar es Salaam.

TUKI (2004) Fasihi ni kazi ya fasihi inayohifadhiwa na kuthibitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Matteru katika TUKI (1983:26) Anaeleza kuwa Fasihi similizi ni aina ya fasihi ambayo hutumia mdomo kuumbwa, kuwasilishwa na kusambazwa kwa wasikilizaji na watumiaji wake. Sanaa hii hutumia Maneno katika mipangilio na amaumbo mbalimbali kutoa dhana ama mawazo Fulani.

Fasihi simulizi yaweza kuelezwa kwamba, hutegemeana. Msanii ambaye huimba kwa amneni katika tukio maalumu (Finnegan, 1970:1-2). Fasihi simulizi inategemea hasa katika utendaji. Oral literature by definition dependent on a performer who formulate it in words on a specific occasion, there is no other way in which it can be realized as a literary product. Oral literature depends on actual performance.

Fasihi simulizi humaanisha Fasihi itolewayo kwa neon la mdomo (Okpewho, 1992:1), anaendelea kusema kuna mbinu mbalimbali ambazo zinatumika katika fasihi simulizi lakini mbinu hizo hazitumiki kwenye fasihi andishi.

Fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa na kuwasilishwa kwa njia yam domo na vitendo bila kutumia Maandishi (Mulokozi 1996:22). Hivyo simulizi na tukio linalofungamana na uktadha(mazingira) Fulani wa kijamii na kutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita fanani (msanii), hadhira, fani inayotendwa, tukio, mahali na wakati.

Oral literature is a perfomed art. Once it is writtern, the live aspects of its performance are lost. Yet these aspects are crucial for a deeper understandings and appreciation if the art (Miruka, 1999:1).

Fasihi simulizi ni sanaa inayohusisha utendaji pale inapowekwa katika maandishi hupoteza utendaji wake. Ambapo uhalisia huu huweza kufanya fasihi simulizi kueleweka kwa ufasaha zaidi na kukubalika kwa hadhira.

Fasihi simulizi ni dhana inayotumika kurejelea kazi mabazo kumsingi hupokezanwa kwa njia ya masimulizi au mdomo.tawi hili la fasihi linatumiwa katika jamii kwa njia ya kupashana maarifa yanayohusu utamaduni Fulani, historia ya jamii, matamanio yao, mtazamo wao na historia yao (Wamitila 2003) katika Nyang'hani (2016:19).

Fasihi simulizi ni sanaa inayobuniwa ikawasilishwa na kusambazwa kwa lugha yam domo. Vyombo vyake vikubwa ni mdomo na sauti ya binadamu katika hali ya kuumba, kusimulia, kuiga, kughani, kutambara, kutega, miradi yote yanatolewa kwa mdomo na ishara za mwili (Mazrui na Symbo. 1992:2),

Kulingana na wataalamu waliotoa fasili mbalimbal za fasihi simulizi kwa ujumla tunaweza kusema kuwa Fasihi simulizi ni aina ya fasihi inayobiniwa na kuwasilishwa kwa hadhira iliyokusudiwa kwa njia ya mazungumzo ambapo huhusisha utendaji na hadhira huonana ana kwa ana na fanani. Kwa mjibu wa wataalamu wafuatao, Matteru 1983, Finnergan 1970, Okpewho 1992, Mulokozi 1996, Miruka 1999, Wamitila 2003 na Mazrui & Syambo 1992. Zifuatazo ni tanzu mbalimbali za fasihi simulizi.

Ngano; ni tungo yoyote ya kubuni inayosimuliwa kwa lugha ya nadhari. Ngano huwa na maneno ya miazno na miisho wakati wa usimulizi mfano:-

Msimulizi: Raukwa

Wasikilizaji: Rakawa

Msimulizi: Hadithi! Hadithi!

Wasikilizaji: Hadithi Njo!

Msimulizi: Hapo zamani za kale…

Ngano inagawanyika katika aina mbalimbali ambazo ni ngano za usuli, ngano za ushujaa, hekaya, hurafa

Nyimbo; kuna nyimbo nyingi katika fasihi ya Kiswahili lakini zilizokusudiwa hapa ni zile zilizotungwa kwamdomo (bila maandishi) na kusambazwa kwa mdomo. Nyimbo hizi hufungamana na ngoma na mara nyingine huimbwa pamoja na muziki.kuna aina mbalimbali za nyimbo mfano bembelezi, nyimbo za watoto, nyimbo za sherehe na taarabu.

Methali; ni misemo mifupi yenye hekima hudhihirisha mkusanyo wa mafunzo waliyopata watu wa vizazi vingi vya jumuiya Fulani katika maisha yao. Methali hutumiwa sana katika mazungumzo ya waswahili na sehemu moja muhimu ya fasihi simulizi Mfano, methali

“Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu”

Vitendawili; ni kauli fupi yenye kusawiri picha ya kimafumbo inayotaka kufumbuliwa au maneno mengine. Vitendawili hutumia lugha yenye mdundo wa kifasihi na tanakali za sauti kitendawili huanza kwa mtega kwa kusema “Kitendawili” ma wasikilizaji waitikia “tega” mtegaji husubiria jibu wanaposhindwa kukitegua husema “nipeni mji” Mfano wa kitendawili “Nyumba haina Mlango”

“_____juu go chini go kati go – go - go_____Ulimi”

Fasihi simulizi kama sanaa inamajukumu kadhaa kwa jamii kama ifuatavyo:-

Huburudisha; fasihi simulizi huweza kutumiwa kama burudani kwenye mkusanyiko wa jammii, tanzu kama hadithi, ushairi, semi kama methali na vitendawili huwaburudisha watu Mfano watoto na hata watu wazima, kwani hadithi, ngano, hekaya huweza kutambwa lama njia ua burudani.

Huelimisha, kupitia fasihi simulizi wanajamii huelimishwa juu ya thamani za kijamii, historia zaoutamaduni na mtazamo wao kiulimwengu toka kizazi kimoja hadi kingine. Mfano kupitia utanzu wa semi hasa methali na vitendawili mfano; mali bila daftari huisah bila habari, methali hii huelimisha juu ya umuhimu wa kutunza umuhimu wa mali zao.

Huifadhi historian a utamaduni wa jamii; fasihi simulizi ni nyenzo muhimu katika kutunza amali za jamii hasa utamaduni pamoja na historia ya jamii Fulani, kwani huwafahamisha wanajamii kifasihi juu ya historia yao, wao ni nani na chimbukolao ni lipi, hivyo fasihi simulizi huisaidia jamii kujielewa na kujitambua.

Fasihi simulizi huunganisha vizazi vya jamii; fasihi simulizi kama msingi mkubwa wa kuwaunganisha wanajamii waliopo na waliotangulia mbele ya haki. Kwani kupitia hadithi za kutambwa, vitendawili, methali na nyimbo zao huwakusanya watu na kuwaweka katika mahusiano yenye mlengo mmoja.

Hufundisha; jamii ina jukumu la kuwafundisha vijana wake maadili ya jamii ile ambayo yana adili yaani funzo au ujumla unaowaelekeza, kuwaadibu, kuwaonya na kuwaongoza katika matarajio ya jamii ile. Hivyo fasihi simulizi kama nyombo za dansi, tenzi, mashairi hutumika kuwafundisha vijana juu ya mienendo mizuri katika jamii yao.

Mfano; Katika vitas ya Kagera 1978, nyimbo za kwaya, nyimbo za mziki wa dansi, tenzi na hata mashairi zilitumika kuhamasisha askari wa Tanzania kumwadhibu adui yetu Nduli Iddi Amini wa Uganda.

Hukuza na kuendeleza stadi za lugha; kwa kuwa fasihi simulizi hutegemea usemi na amamko katika kusimulia hadithi, hutegemea vitendawili na hata kuimba hivyo fasihi simulizi ina mchango mkubwa wa kuboresha uwezo wetuj wa kuzimudu stadi za kugha.

Mfan;kusikiliza na hata kuongea, pia fasihi simulizi imechangia pakubwa katika fasihi andishi kwani kilichiandikwa kimetokana na fasihi simulizi, hivyo fasihi simulizi ni msingi wa fasihi andishi.

Hukuza umoja na ushirikiano miongoni mwa wanajamii, ilivyo ni kwamba fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima na sio mtu binafsi, hadithi zinaposimuliwa kwa hadhira kubwa, vitendawili vinapotegwa kwenye kundi kubwa na kwa sababu kimsingi fasihi simulizi ndivyo ilivyokusudiwa itumike katika muktadha wa kuvihusisha sio vikundi vidogo vidogo tu bali hata jamii nzima.

Kwa ujumla fasihi simulizi kama utanzu wa kisanaa una manufaa makubwa miongoni mwa wanajamii hasa kupitia tanzu zake kama hadithi, semi, maigizo, ushairi na hata mazungumzo, kwani husaidia jamii kujielewa na kujitambua juu ya maisha yao kulingana na wakati Fulani kwa maendeleo ya kiuchumi.